



# NISHATI

HABARI ZA  
NISHATI

## News *Bulletin*

[www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz) [Wizara ya Nishati](https://www.facebook.com/Wizara ya Nishati) [wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](https://www.instagram.com/wizara_ya_nishati_tanzania) [@Nishati2017](https://twitter.com/Nishati2017) [Wizara ya Nishati](https://www.youtube.com/Wizara ya Nishati)

Toleo Namba 30

Septemba 1 - 30, 2021

# RAIS SAMIA APONGEZWA UTEKELEZAJI MIRADI YA UMEME VIJIJINI



LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA  
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au  
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma

# RAIS SAMIA APONGEZWA UTEKELEZAJI MIRADI YA UMEME VIJIJINI

**Veronica Simba na  
Zuena Msuya -  
Manyara\***

**V**iongozi mbalimbali akiwemo Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Wabunge wa Majimbo yaliyopo Wilaya ya Mbulu na Mkuu wa Wilaya hiyo, Sezaria Makota, wamempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu kwa utekelezaji makini wa miradi ya umeme vijijini.

Walitoa pongezi hizo kwa nyakati tofauti wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Manyara, iliyofanyika Agosti 14 mwaka huu, kijiji cha Mongahay, Kata ya Tumati, wilayani Mbulu.

Akizungumza na

wananchi kabla ya kuzindua rasmi Mradi huo, Naibu Waziri Byabato alisema kuwa Rais Samia, kupitia Serikali ya Awamu ya Sita anayoiongoza, amewezesha upatikanaji wa fedha za kutosha kwa ajili ya kuhakikisha vijiji vyote ambavyo havijafikishiwa umeme vinapelekwa nishati hiyo kabla ya Desemba 2022.

Byabato alitumia jukwaa hilo kutoa rai kwa wananchi kuchangamkia fursa ya kufikiwa na miundombinu ya umeme katika maeneo yao kwa kuhakikisha wanalipia shilingi 27,000 tu ili waunganishiwe na kuutumia katika shughuli mbalimbali za maendeleo ili kuboresha maisha yao.

“Mheshimiwa Rais ametuwezesha tukawaletea umeme, niwaombe Waheshimiwa Wabunge mhamasishe

wananchi wenu wakimbilie fursa hii ili iwalettee maendeleo.”

Akifafanua, Naibu Waziri alieleza kuwa katika baadhi ya maeneo ambayo yaefikishiwa miundombinu ya umeme, mwitikio wa wananchi kulipia ili kuunganishiwa nishati hiyo, umekuwa mdogo, jambo alilolieleza kuwa ni kurudisha nyuma jitihada za Serikali za kuwaletea wananchi maendeleo.

“Serikali inatumia gharama kubwa kuhakikisha miundombinu ya umeme inatufikia. Sasa, miundombinu ikifika kwenye maeneo yetu, tuhakikishe sisi sote tunahamasishana kuchangamkia fursa hiyo,” alisisitiza Naibu Waziri Byabato.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Sezaria Makota alipongeza kazi kubwa inayoendelea kufanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kusambaza umeme vijijini huku

mkazo kuwa vijiji vyote vya Wilaya hiyo, ambavyo havijafikiwa na umeme, vimeingia katika kufikishiwa nishati hiyo kupitia Mradi huo uliozinduliwa siku hiyo.

Naye Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mji, Zacharia Issaay alieleza kuwa kazi ya kusambaza umeme vijijini iliyofanywa na Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ni ya kupongezwa sana kwani imesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha maisha ya wananchi.

“Nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano na ya Sita kwa kazi kubwa ya usambazaji umeme vijijini kupitia REA.”



# RAIS SAMIA APONGEZWA UTEKELEZAJI MIRADI YA UMEME VIJIJINI

Mbunge Issaay alibainisha kuwa kadri umeme unavyounganishwa katika maeneo mbalimbali ndivyo wananchi wengi wanavyohamasika kufungua miradi ya kimaendeleo zikiwemo mashine za kusaga

nafaka, hivyo akaiomba Serikali kuongeza wigo wa upelekaji huduma hiyo kwa manufaa ya jamii husika.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini, Fratei Massay alimwomba Naibu Waziri Byabato kufikisha

salamu za wananchi wa eneo hilo alizozita 'za kindakindaki' kwa Rais Samia kutokana na kazi kubwa anayoifanya ya kuwapelekea maendeleo ikiwemo umeme.

"Naishukuru Serikali kwenye Bajeti hii iliyopita, tumepata vijiji karibu vyote kasoro kimoja tu. Ukikosa kimoja haulalamiki bali unashukuru," alisisitiza Masai.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Amos Maganga alibainisha kuwa Mkoa wa Manyara una jumla ya vijiji 441 ambapo vijiji 278 tayari vina umeme na vilivyosalia 163 vinapelekewa nishati hiyo kupitia Mradi wa

Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili.

Kwa upande wa Wilaya ya Mbulu, Mhandisi Maganga alieleza kuwa kuna jumla ya vijiji 110 ambapo vyenye umeme ni 48.

Alifafanua kuwa vijiji vitakavyopelekewa umeme kupitia Mradi huo wa Awamu ya Pili ni 62 na kwa gharama ya shilingi bilioni 18.8.

Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili kwa Mkoa wa Manyara unatekelezwa na Kampuni ya Ukandarasi ya Nakuroi Investment pamoja na Giza Cable Industries Ltd kwa gharama ya shilingi bilioni 65.3.



# WALIOZEMBEA AJALI YA MOTO MSAMVU WACHUKULIWE HATUA KALI\_ WAZIRI MKUU

**Na Teresia Mhagama**

**W**aziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, ameagiza kuwa, hatua kali zichukuliwe kwa Wataalam kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) waliozembea na kupelekea baadhi ya mitambo ya umeme katika kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Msamvu kuungua moto.

Waziri Mkuu ametoa maagizo hayo tarehe 14 Agosti, 2021 mkoani Morogoro wakati alipokagua athari zilizotokea baada ya kutokea hitilafu iliyopelekea kituo hicho kuwaka moto Agosti 2, 2021 ambapo aliambatana na viongozi mbalimbali wakiwemo Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, Naibu Katibu Mkuu, Kheri Mahimbali, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro,



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, akitambulisha viongozi wa Wizara ya Nishati wakati Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa alipofika katika kituo cha umeme cha Msamvu mkoani Morogoro kuangalia athari zilizotokea baada ya kituo hicho kuungua moto.*



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, akiwa katika chumba cha kuendesha mitambo ya umeme katika kituo cha umeme cha Msamvu ambacho kilipata athari baada ya kituo kuungua moto. Kushoto ni Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani.*

Martin Shigella, Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Edward Ishengoma na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dkt. Tito Mwinuka.

“Hatua ambayo umeshaichukua Waziri wa Nishati ya kuwasimamisha wataalam waliofanya uzembe, naipongeza kwa sababu kama mfumo ulikuwa unaonyesha kuna hitilafu na wataalam walilazimisha kurudisha umeme, huku wakijua hatari iliyopo, haya ni makusudi ambayo yameleta matatizo kwenye mitambo hii ya umeme na hii ni hasara kubwa.” Amesema Waziri

Mkuu

Ameongeza kuwa “Wayanaoleta umeme kwenye kituo hiki imeelezwa kuwa haukufukiwa kwa kina kinachotakiwa na hivyo kupelekea a kukatwa na greda linalotumika katika mradi wa SGR, nakupongeza Waziri kwa kumsimamisha pia msimamizi wa TANESCO anayetakiwa kuhakikisha kuwa nyaya hizi zinafukiwa kwa kina kinachotakiwa, pia kama kuna mtaalam mwingine anahusika, endelea kuchukua hatua.”

Ameagiza kuwa wataalam hao wakibainika kuwa wamefanya makosa, wachukuliwe hatua kali ili iwe funzo kwa

# WALIOZEMBEA AJALI YA MOTO MSAMVU WACHUKULIWE HATUA KALI\_WAZIRI MKUU

wengine kwani matukio kama hayo yanaweza kujitokeza pia katika mikoa mingine.

Aidha amewakumbusha wataalam wa TANESCO katika vituo vya kupoza umeme kutunza mitambo hiyo na wahakikishe kuwa kila kitu kinasimamiwa kwa weledi na umakini mkubwa ili kuepusha uzembe utakaopelekea hasara ikiwemo ya kuunguza vifaa vya wananchi.

Pia ameeleza kuwa



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, akiwa katika kituo cha umeme cha Msamvu mkoani Morogoro ambapo alifika ili kukagua athari zilizotokea baada ya kituo hicho kuungua moto. Wengine katika picha ni viongozi mbalimbali wakiwemo Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kulia kwa Waziri Mkuu) na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martin Shigella (kushoto kwa Waziri Mkuu).



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, akiwa katika kituo cha umeme cha Msamvu mkoani Morogoro ambapo alifika ili kukagua athari zilizotokea baada ya kituo hicho kuungua moto. Wengine katika picha ni viongozi mbalimbali wakiwemo Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kulia kwa Waziri Mkuu) na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martin Shigella (kushoto kwa Waziri Mkuu).

kwa sasa wananchi mkoani Morogoro wanalalamika kuhusu changamoto ya upatikanaji umeme wa uhakika ikiwemo viwanda vilivyopo mkoani humo, hivyo amemwagiza Waziri wa Nishati kufuatilia kazi ya upelekaji wa transfoma nyingine katika kituo hicho ili ianze kazi mara moja.

Awali, Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani alimweleza Waziri Mkuu kuwa, wataalam watano

wamesimamishwa ili kupisha uchunguzi na taarifa ya uchunguzi huo itawasilishwa tarehe 15 Agosti, 2021.

Aidha alieleza kuwa, ameshawaagiza TANESCO kufunga mifumo itakayobaini hitilafu moja kwa moja mara inapotokea badala ya kutegemea wataalam wanaosimamia miundombinu ya umeme kuanza kutembea ili kutafuta chanzo cha hitilafu ya umeme pale inapotokea.

# Waziri wa Nishati azindua matumizi ya Gesi Asilia katika nyumba 300 Mtwara



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wananchi katika mtaa wa Kyangu (Hawapo pichani) wakati wa hafla ya kuzindua matumizi ya Gesi Asilia katika nyumba 300 wilayani Mtwara.

## Na Teresia Mhagama,

**W**aziri wa Nishati, Dkt. Medard

Kalemani amezindua matumizi ya Gesi Asilia majumbani katika nyumba 300 ambazo zimeunganishwa na nishati hiyo wilayani Mtwara kwa gharama ya shilingi milioni 961.7

Uzinduzi huo ulifanyika tarehe 25 Agosti, 2021 katika Mtaa wa Kyangu wilayani Mtwara, na kuhudhuriwa na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Viongozi mbalimbali katika Mkoa wa Mtwara wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya

ya Mtwara, Dunstan Kyobya, Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Adam Zuberi, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Khalfan Khalfan, Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunjje.

“ Hii ni awamu ya Pili ya usambazaji Gesi Asilia majumbani katika Mkoa wa Mtwara kwani katika awamu ya kwanza wateja takriban 125 waliunganishwa na wananufaika na gesi hii katika mitaa ya Reli A na B, Kyangu, Masandube na Lilungu.” Alisema Dkt. Kalemani

Ili kuhakikisha nishati hiyo inawafikia wananchi wengi zaidi, aliagiza TPDC na kampuni yake tanzu inayohusika na usambazaji wa Gesi Asilia (GASCO), kusambaza gesi hiyo kwa wananchi wote bila kubagua kutokana na manufaa yake mbalimbali kama vile unafuu wa gharama kulinganisha na nishati nyingine zinazotumika kupikia, pia inapunguza uharibifu wa mazingira.

Aidha, alieleza kuwa matumizi ya Gesi Asilia mkoani humo yasiishie tu kwenye Taasisi na majumbani, hivyo ameagiza TPDC kufungua kituo cha kujazia gesi kwenye

magari na kwenye viwanda mbalimbali.

Vilevile, Waziri wa Nishati aliagiza TPDC, kuendelea kutumia vifaa vinavyotengenezwa ndani ya nchi katika shughuli za usambazaji Gesi Asilia majumbani na kueleza kwa kufanya hivyo kutaleta manufaa mbalimbali ikiwemo kuongezeka kwa ajira na uhakika wa upatikanaji wa vifaa.

Aliongeza kuwa lengo la Serikali sasa ni kupeleka Gesi Asilia hadi vijijini kupitia mpango wa usambazaji nishati vijijini, hivyo aliwaagiza TPDC kuendelea kuwahamasisha wananchi kutumia



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizungumza na wananchi katika mtaa wa Kyangu (Hawapo pichani) wakati wa hafla ya kuzindua matumizi ya Gesi Asilia katika nyumba 300 wilayani Mtwara tarehe 25 Agosti, 2021.

# Waziri wa Nishati azindua matumizi ya Gesi Asilia katika nyumba 300 Mtwara



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Meya wa Manispaa ya Mtwara, Shadida Ndile, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya, Mwenyekiti wa Bodi ya TPDC, Khalfan Khalfan wakiwa katika picha ya pamoja na Wafanyakazi wa Kampuni ya usambazaji Gesi (GASCO) mara baada ya kuzindua matumizi ya Gesi Asilia katika nyumba 300 wilayani Mtwara tarehe 25 Agosti, 2021. Nyuma ya Waziri wa Nishati ni Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, James Mataragio.

nishati hiyo.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, alieleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita itahakikisha kwa Gesi Asilia iliyopo inawanufaisha wananchi mkoani Mtwara na watazania kwa ujumla.

Kuhusu maagizo mbalimbali yaliyotolewa na Waziri wa Nishati, alieleza kuwa atahakikisha yanatekelezwa kwa ufanisi kwa kushirikiana na Taasisi zilizo chini ya Wizara zinazohusika na

nishati hiyo.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, James Mataragio alisema kuwa kazi ya usambazaji Gesi Asilia majumbani ni endelevu kwani katika mwaka 2021/22 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuunganisha nishati hiyo katika nyumba nyingine 300.

Kuhusu mradi wa usambazaji Gesi Asilia majumbani wa Awamu ya Pili, alieleza kuwa umetekelezwa na wataalam wa ndani ambao ni wahandisi watazania kutoka

kampuni ya GASCO tofauti na mradi wa Awamu ya kwanza ambao ulitumia wakandarasi na hivyo



Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya akizungumza na wananchi katika mtaa wa Kyangu (Hawapo pichani) wakati wa hafla ya kuzindua matumizi ya Gesi Asilia katika nyumba 300 wilayani Mtwara tarehe 25 Agosti, 2021.

gharama zake zilikuwa juu tofauti na mradi wa Awamu ya Pili.

Alifafanua kuwa, mradi wa Awamu ya Kwanza ulitumia katribani shilingi Bilioni 3.2 huku mradi wa Awamu ya Pili ukitumia shilingi milioni 961.7 hivyo Serikali imekoa fedha takriban shilingi Bilioni 2.

Alisema kuwa, Mji wa Mtwara ni mojawapo ya miji ambayo kwa sasa inanufaika na matumizi ya Gesi Asilia kwani mji huo umeunganishwa na miundombinu yenye jumla ya km 56.7 inayopeleka gesi kwa matumizi ya kuzalisha umeme, wateja wa majumbani, Taasisi na kiwanda cha Dangote.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Meya wa Manispaa ya Mtwara, Shadida Ndile, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya, Mwenyekiti wa Bodi ya TPDC, Khalfan Khalfan wakiwa katika picha ya pamoja na Wafanyakazi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) mara baada ya kuzindua matumizi ya Gesi Asilia katika nyumba 300 wilayani Mtwara tarehe 25 Agosti, 2021.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Meya wa Manispaa ya Mtwara, Shadida Ndile, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya, Mwenyekiti wa Bodi ya TPDC, Khalfan Khalfan wakiwa katika picha ya pamoja na viongozi kutoka Taasisi mbalimbali waliohudhuria hafla kuzindua matumizi ya Gesi Asilia katika nyumba 300 wilayani Mtwara tarehe 25 Agosti, 2021.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, wakikata utepe katika nyumba ya Bi. Magreth James, ikiwa ni ishara ya kuzindua matumizi ya Gesi Asilia katika nyumba 300 wilayani Mtwara tarehe 25 Agosti, 2021.



# SERIKALI YAIAGIZA TIPER KUTOA TAARIFA ZA UENDESHAJI KAMPUNI KWA WAKATI

**Na Dorina G. Makaya – Dar-es-salaam**

**S**erikali imeiagiza Kampuni ya Uhifadhi Mafuta (TIPER) kuhakikisha inatoa taarifa za uendeshaji wa kampuni hiyo kwa wakati, ili kuepusha changamoto ambazo zinaweza kujitokeza baadaye kutokana na kutokutoa taarifa kwa wakati.

Agizo hilo lilitolewa



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali akizungumza na Waandishi wa Habari wakati alipotembelea Kampuni ya Uhifadhi Mafuta (TIPER) iliyopo jijini Dar-esalaam tarehe 31 Julai, 2021 kujionea hali halisi ya uendeshaji wa kampuni hiyo.*

jijini Dar-esalaam tarehe 31 Julai, 2021 na Naibu Katibu Mkuu

wa Wizara ya Nishati Kheri Mahimbali wakati wa ziara yake kwenye

kampuni hiyo iliyolenga kujionea hali halisi ya uendeshaji wa kampuni ya TIPER.

Katika ziara yake, Naibu Katibu Mkuu Mahimbali, alitembelea kwenye maeneo mbalimbali ya kampuni hiyo ikiwa ni pamoja na matenki ya kuhifadhia mafuta jambo ambalo alionyesha kuridhishwa na utendaji kazi wa kampuni hiyo.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Uhifadhi Mafuta (TIPER) Michael Mjinja, aliishukuru Serikali kwa kufika katika eneo hilo ambapo wameweza kukubaliana masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupeana taarifa kwa wakati.

Alisema, licha ya mafanikio waliyonayo, bado kuna changamoto zinazowakabili huku kubwa ikiwa kuharibika kwa vifaa vya kusukuma mafuta pindi wanapoyatoa kwenye meli, vifaa ambavyo havipatikani nchini hadi viagizwe nje ya nchi.

Kufuatia hali hiyo, Naibu Katibu Mkuu wa



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Uhifadhi Mafuta (TIPER) Michael Mjinja wakati alipotembelea Kampuni hiyo iliyopo jijini Dar-esalaam tarehe 31 Julai, 2021 kujionea hali halisi ya uendeshaji wa kampuni hiyo.*

# SERIKALI YAIAGIZA TIPER KUTOA TAARIFA ZA UENDESHAJI KAMPUNI KWA WAKATI



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Uhifadhi Mafuta (TIPER) Michael Mjinja akitoa maelezo kuhusu utendaji wa Kampuni ya TIPER kufuatia ziara ya Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali kwenye kampuni hiyo tarehe 31 Julai, 2021.



Watumishi wa Kampuni ya Uhifadhi Mafuta (TIPER) wakimsikiliza Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali alipokuwa akizungumza nao (Hayumo pichani) alipotembelea kampuni hiyo ya TIPER tarehe 31 Julai, 2021.

Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali alisema, endapo taarifa hizo zitatolewa mapema, itakuwa mwarobaini wa changamoto hizo.

Ziara hiyo ni mwanzo wa ziara nyingine katika taasisi zote zenye ubia na Serikali katika Sekta ndogo ya Mafuta hapa nchini kwa lengo la kuboresha ufanisi na utendaji.

Katika ziara hiyo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Kheri Mahimbali, aliambatana na baadhi ya viongozi na wataalam kutoka Wizara ya Nishati, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji Nchini Tanzania (EWURA) na Kampuni ya Serikali ya Uagizaji na Usambazaji wa Mafuta nchini (TANOIL).

# Watatu wasimamishwa kazi, Kamati yaundwa kuchunguza moto Msamvu

## Na Zuena Msuya

**W**aziri wa Nishati, Dkt. Medard

Kalemani amewasimamisha kazi wahandisi watatu wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kupisha uchunguzi baada ya Kituo cha Kupoza na Kusambaza Umeme Msamvu kuungua moto na kusababisha hasara ya takribani shilingi Bilioni 2.

Aidha amemuagiza Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Kheri Mahimbali kuunda

kamati ya kuchunguza na kubaini chanzo halisi cha Moto huo na hasara iliyopatika ndani ya siku tano kuanzia leo (Agosti 3, 2021).

Katika ziara hiyo, Dkt. Kalemani aliambatana na Naibu Katibu Mkuu wizara hiyo, Kheri Mahimbali, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Edward Ishengoma, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dkt. Tito Mwinuka pamoja na viongozi wengine waandamizi wa Wizara na TANESCO.

Sambamba na hilo aliagiza Kampuni ya inayotekeleza Mradi wa Reli ya Umeme (SGR) kumchungumza



Sehemu ya mitambo iliyoungua katika kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Msamvu mkoani Morogoro, Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani na ujumbe wake walifanya ziara ya kukagua athari za moto katika kituo hicho Agosti 03, 2021.

mhandisi wake anayedaiwa kusababisha hitilafu hiyo kwa kukata waya wa umeme na kari la kuchimbua barabara wakati akitekeleza majukumu yake na

kuchukuliwa hatua pindi itakapobainika.

Dkt. Kalemani alisema hayo, Mkoani Morogoro, Agosti 03, 2021 alipofanya ziara ya kukagua kituo cha



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kushoto) na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (katikati) wakikagua sehemu ya mitambo iliyoungua katika Kituo cha Kupoza na Kupoza umeme cha Msamvu mkoani Morogoro, Agosti 03, 2021.



Moja ya Miundombinu ya umeme iliyoungua katika Kituo cha Kupoza na Kupoza umeme cha Msamvu mkoani Morogoro, Waziri wa Nishati alifanya ziara ya kukagua kituo hicho Agosti 03, 2021.

# Watatu wasimamishwa kazi, Kamati yaundwa kuchunguza moto Msamvu



Mafundi wakiendelea na kazi ya ukarabati katika Kituo cha Kupokea na Kupoza umeme cha Msamvu mkoani Morogoro baada ya kuungua ili kurejesha kituo hicho katika hali yake ya kawaida, Waziri wa Nishati alifanya ziara ya kukagua kituo hicho Agosti 03,2021.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (wa pili kulia) na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (wa pili kushoto) wakikagua waya mkubwa unaodaiwa kukatwa na aliyekuwa akikwangua barabara na kusababisha kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Msamvu mkoani Morogoro kuungua moto, ziara ilifanyika Agosti 03,2021.

Kupoza na Kusambaza Umeme cha Msamvu kilichoungua moto Jana baada ya kutokea hitilafu na kusababisha wananchi kukosa Umeme.

Dkt. Kalemani alifafanua kuwa wahandisi hao wa TANESCO, wamesimamishwa kwa kushindwa kubaini hitilafu iliyotokea katika mifumo ya kuendesha mitambo kituoni hapo, na kusababisha harasa kubwa kwa taifa baada ya kituo hicho kuungua moto.

“Wahandisi waliokuwa zamu siku hiyo wasimamishwe kazi kuanzia Sasa kwa kushindwa kubaini mapema hitilafu iliyotokea katika mifumo na kusababisha hasara kubwa kwa Taifa, wakati walikuwepo kazini, pia matukio ya moto yamekuwa mengi lazima tuchunguze kufahamu kama kuna yeyote anahujumu miundombinu ya umeme”, alisema Dkt. Kalemani

Hata hivyo aliitaka TANESCO kufanya

# Watatu wasimimishwa kazi, Kamati yaundwa kuchunguza moto Msamvu

kazi usiku na mchana kuhakikisha umeme unarejea katika maeneo yote ndani ya saa 24 kuanzia leo, vilevile waongeze wataalam kutoka vituo vingine ili kuongeza nguvu kazi na kukamilisha kazi hiyo haraka.

Aidha Dkt. Kalemani aliwataka TANESCO kuharakisha manunuzi ya vifaa na miundombinu yoyote iliyongua

kwa kutumia mfumo wa dharura usioathiri taratibu za manunuzi ili kurejesha kituo hicho katika hali yake ya kawaida ndani ya kipindi kifupi.

Vilevile aliwata TANESCO kuhakikisha kuwa vituo vyote vya vilivyojenga zamani za kupoza na kusambaza umeme vinakuwa na mifumo maalum ya kubaini hitalafu ikitokea

na namna ya kuidhibiti kabla ya madhara makubwa kutokea.

Pamoja na mambo mengine aliwaagiza kuweka alama katika maeneo yote ambayo miundombinu mikubwa ya umeme imepita chini ya ardhi hasa nyaya ili kutoa tahadhari kwa watakaokuwa wakifanya kazi au kupita maeneo hayo.

Pamoja na mambo

mengine aliwataka wananchi ambao bado huduma ya umeme haijarejea kuendelea kuvuta subira wakati wataalam wakiendelea kufanya kazi zao, na kwamba tayari baadhi ya vifaa kutoka mkoani Singida viko njiani kuwasili eneo hilo ili kuhakikisha huduma ya umeme inarejea maeneo yote ndani ya muda mfupi.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kulia) na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (katikati) na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martin Shigela wakitoka kukagua eneo linalodaiwa kuwa chanzo cha hitilafu iliyosababisha Kituo cha Kupokea na Kupoza umeme cha Msamvu, mkoani Morogoro kuungua moto, ziara ilifanyika Agosti 03, 2021.

## SERIKALI IMETOA BILIONI 259.96 KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA

**Na Dorina Makaya - Chato, Geita.**

**S**erikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa kiasi cha shilingi bilioni 259.96 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Mafuta.

Hayo yalielezwa na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani wakati akizungumza na wananchi wa Kata

ya Bukome, Kijiji cha Nyakato, Wilayani Chato Mkoani Geita tarehe 10 Agosti, 2021.

Waziri Kalemani aliwataka wananchi hao kuchangamkia fursa mbalimbali za ujenzi wa bomba la mafuta litakalopita katika mikoa 8 ya Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga.

Waziri Kalemani alizitaja fursa hizo kuwa



*Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akiwasisitiza wananchi wa wilaya Chato kuchangamkia fursa ya ujenzi wa bomba la mafuta litakalojengwa kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani Tanga-Tanzania wakati wa Mkutano wa wananchi na wadau kuhusu fursa za Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki tarehe 10 Agosti, 2021 Mkoani Geita.*



*Baadhi ya washiriki wa Mkutano wa wananchi na wadau kuhusu fursa za Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 10 Agosti, 2021 mkoani Geita wakifuatilia kwa makini hotuba ya Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani (Hayumo pichani) wakati wa mkutano huo.*

## SERIKALI IMETOA BILIONI 259.96 KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA



Mwakilishi wa Mkuu wa mkoa wa Geita ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Chato, Martha Mkupasi akiwasisitiza wananchi (hawamo pichani) kutunza miundombinu ya bomba la mafuta ambayo itapita kwenye maeneo yao.

Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani (Katikati) akikabidhi hundi kwa wananchi waliopisha maeneo yao kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi.

ni pamoja na usafirishaji, ulinzi, chakula, vinywaji, huduma ya malazi na mafuta kwa ajili ya magari na mitambo.

Alizitaja fursa nyingine kuwa ni pamoja na shajala, bidhaa za ujenzi zinazopatikana hapa nchini, shughuli

za ujenzi, huduma za mawasiliano na ukodishwaji wa mitambo ya ujenzi.

Dkt. Kalemani alieleza kuwa Jumla ya shilingi bilioni 28 zinategemea kulipwa kwa wananchi waliopitiwa na bomba la mafuta kutoka Hoima

nchini Uganda hadi Chongoleani Tanga nchini Tanzania.

Aidha, Waziri Kalemani alisema, mradi wa ujenzi wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi utanza kutekelezwa ifikapo Septemba 2021.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa

wa Geita, Rosemary Senyamule, Mkuu wa Wilaya ya Chato Martha Mkupasi aliwataka wananchi kutunza miundombinu ya bomba la mafuta ambayo itapita kwenye maeneo yao.



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akifurahi pamoja na wananchi wa Nyakato, Wilaya ya Chato ambao wamekubali kupisha maeneo yao kwa ajili ya ujenzi wa bomba la mafuta ghafi.

# Byabato: Atakayekwamisha usambazaji Umeme Vijijini, hataachwa salama!

**Veronica Simba na  
Zuena Msuya- Manyara**

**N**aibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato amesema yeyote atakayekwamisha kazi ya kusambaza umeme vijijini atachukuliwa hatua kali za kisheria na kinidhamu kwakuwa anarudisha nyuma juhudi za serikali kupeleka maendeleo kwa wananchi.

Wakili Byabato amesema hayo Agosti 14, 2021 wakati akizindua mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Manyara. Hafla ya uzinduzi



*Naibu wa Waziri Wakili Stephen Byabato, akizungumza wakazi wa Kijiji cha Mungahay, Kata ya Tumati, wakati akizindua mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Manyara uliofanyika Wilayani ya Mbulu, Agosti 14, 2021.*

huo imefanyika katika Wilaya ya Mbulu ambapo amewasha umeme katika Kijiji cha Mungahay, Kata ya Tumati.

Akizungumza na wananchi waliohudhuria uzinduzi huo, Naibu Waziri amesema kuwa Serikali imetenga

fedha nyingi kwa ajili ya kuhakikisha kuwa vijiji na vitongoji vyote nchini vinapata umeme kabla ya Desemba 2022,



*Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga akizungumza wakazi wa Kijiji cha Mungahay, Kata ya Tumati, wakati uzinduzi wa Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Manyara uliofanyika Wilayani ya Mbulu, Agosti 14, 2021.*



*Naibu wa Waziri Wakili Stephen Byabato, (katikati) na baadhi ya Wananchi wakifurahi baada ya kukata utepe wakati wa wakati akizindua mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Manyara uliofanyika Wilayani ya Mbulu, katika Kijiji cha Mungahay, Kata ya Tumati, Agosti 14, 2021.*



# Byabato: Atakayekwamisha usambazaji Umeme Vijijini, hataachwa salama!

hivyo haitavumilia kuona mtu yeyote anathubutu kukwamisha kazi husika.

“Hatutamwacha salama mtu yeyote awe Mkandarasi, Afisa kutoka TANESCO, Wizara ya Nishati na hata mwananchi. Lazima tutamshughulikia. Hilo nawaambia wazi,” amesisitiza Wakili Byabato.

Akizungumzia Mkoa wa Manyara, Byabato amesema kuwa Serikali imetenga kiasi cha shilingi Bilioni 65.3 zitakazotumika kusambaza umeme katika vijiji vyote 163 vilivyosalia katika Mkoa huo.

Aidha, amebainisha kuwa Kampuni mbili za Wakandarasi ndizo zilizoshinda kutekeleza Mradi huo wa kusambaza umeme katika wilaya zote tano za Mkoa huo ambazo ni Kiteto, Mbulu, Babati, Simanjiro na Hanang.

Amezitaja Kampuni hizo kuwa ni Nakuroi ambayo itatekeleza mradi huo katika Wilaya ya Mbulu, Hanang na Babati na kuunganisha umeme katika vijiji 138 vya wilaya hiyo kwa gharama ya shilingi



*Wanafunzi wa Shule ya Msingi, Munguhay na baadhi ya Wananchi wakifurahi wakati Wakamsikiliza Naibu waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (hayupo pichani) wakati akizindua mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Manyara uliofanyika Wilayani ya Mbulu, katika Kijiji cha Munguhay, Kata ya Tumati, Agosti 14, 2021.*

Bilioni 35.

Kampuni nyingine ni Giza itakayotekeleza Mradi katika Wilaya ya Kiteto na Simanjiro ambapo itaunganisha jumla ya vijiji 42 kwa wilaya hizo kwa gharama ya shilingi Bilioni 30.

Sambamba na hilo, Wakili Byabato amewataka wananchi hao kutandaza nyaya katika nyumba zao na kulipia gharama ya shilingi 27,000 tu pasipo kulipishwa gharama za nguzo, nyaya pamoja na mita.

Amewataka wananchi hao kutoa taarifa katika ofisi za

Serikali za Mitaa, Kata, Wilaya, Mkoa pamoja na TANESCO, pale mtu yeyote atakapomtaka mwananchi kulipia miundombinu yoyote ya umeme ili aunganishiwe huduma hiyo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga amewataka wananchi hao kuwa walinzi wa miundombinu ya umeme katika maeneo yao pamoja na kutoa ushirikiano kwa wakandarasi wanaotekeleza mradi huo.

Vilevile

Mhandisi Maganga amewahamasisha wananchi hao kuchangamkia fursa ya kufanya kazi zisizohitaji taaluma maalum, ili waweze kujiongeza kipato na kufurahia uwepo wa mradi huo katika maeneo yao.

Amewakumbusha wakandarasi waliopewa kazi ya kutekeleza mradi huo kuwa Serikali haitaongeza muda kwa mkandarasi yeyote atakayechelewa kukamilisha mradi huo kwa wakati na kwamba atakatwa asilimia kumi (10%) ya malipo yake.

# Dkt. Kalemani apiga marufuku upandishaji wa bei ya gesi nchini

**Hafsa Omar-  
Dodoma**

**W**aziri wa Nishati, Dkt. Medard

Kalemani amewapiga marufuku wauzaji na wasambazaji wa Gesi za majumbani kupandisha bei ya bidhaa hiyo.

Amepiga marufuku hiyo Agosti 18, 2021, Jijini Dodoma alipofanya ziara ya kushtukiza kwenye maduka mbalimbali kwa wauzaji wa gesi hiyo.

Dkt. Kalemani alisema kuwa, Serikali haitakubali kuona wafanyabiashara wanajipangia bei kubwa ambazo zinawaumiza Watanzania.

“Ninawapa onyo la mwisho wafanyabiashara wote wa gesi za majumbani kutopandisha bei, pia Mamlaka ya Udhhibiti Huduma za Nishati na Maji (EWURA) walishatoa maelekezo, Mimi Waziri wa Nishati napita sasa kutoa onyo la mwisho, tukirejea

wakati mwingine na kukuta bei imepanda tutachukua hatua ikiwa ni pamoja na kukufungia biashara husika kwa mtuhumiwa”, alisisitiza Dkt.Kalemani.

Alifafanua kuwa, Mtungi wa ujazo wa kilo 6 unatakiwa kuuzwa kati ya shilingi 20, 000 hadi shilingi 21,000 na Mtungi wa ujazo wa kilo 15 unauzwa kati ya shilingi 47,000 hadi shilingi 50,000 na bei hiyo ni kwa wauzaji wa jumla na rejareja.

Aidha, alisema kuwa Serikali inafahamu bei ya gesi katika soko la dunia imepanda lakini si kwa kiasi kikubwa ambacho inawafanya wafanyabiashara kupandisha bei ya bidhaa hiyo hata kuliko namna ilivyopanda katika soko la dunia.

“Serikali inaendelea kufuatilia bei ya Soko la dunia na kama bei itapanda sana mtaelekezwa na kupewa utaratibu na EWURA lakini kwasasa

haitapanda hatutaki kuleta kero kwa wananchi alisema”, alisema Dkt. Kalemani.

Hata hivyo, aliwataka wafanyabiashara hao endapo watapata changamoto yoyote wawasiliane na EWURA ili waweze kupewa utaratibu unaotakiwa.

Pia, aliwaagiza Mamlaka ya Udhhibiti Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kuchukua hatua kali kwa yoyote ambae atakiuka maagizo hayo.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akizungumza na muuzaji wa Gesi za Majumbani, Yona Kesi (kushoto) wakati alipofanya ziara ya kushtukiza kwenye maduka mbalimbali kwa wauzaji wa Gesi za Majumbani, kulia Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuber, ziara hiyo ilifanyika Agosti 18, 2021, jijini Dodoma.

# Wakili Byabato - Waliobadilishiwa TARRIF watoe taarifa TANESCO zirekebishwe



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, akizungumza na wananchi wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wakulima nchini maarufu kama Nane Nane kwa Mkoa wa Kagera yaliofanyika katika Uwanja wa Kyakailabwa, wilayani Bukoba Mkoani humo, Agosti 8, 2021.

Na Zueni Msuya  
Kagera,

**N**aibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato amesema watumiaji wa Umeme Waliobadilishiwa Tozo za kutoa huduma (TARRIF) kutoka kundi moja kwenda jingine pasipo wao kubadilisha matumizi halisi watoe taarifa katika Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ili kufanyiwa marekebisho ya tozo

hizo.

Wakili Byabato alisema hayo wakati akifunga Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wakulima nchini maarufu kama Nane Nane kwa Mkoa wa Kagera yaliofanyika katika Uwanja wa Kyakailabwa, wilayani Bukoba Mkoani humo, Agosti 8, 2021.

Aidha aliwataka TANESCO kuhakikisha wanarekebisha TARRIF kwa makundi yote ya watumiaji wa umeme kulingana na matumizi husika ili kuondoa malalamiko kwa wateja.

“Kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wateja wa umeme, kuhusu kubadilishiwa TARRIF katika matumizi ya Umeme, pasipo wateja hao kubalisha matumizi yao halisi, wateja wa namna hiyo wanapotoa taarifa TANESCO washughulikiwe haraka iwezekanavyo na warudishiwe katika TARRIF za matumizi yao halisi, na kama matumizi ya mteja yamezidi kiwango cha awali cha TARRIF afahamishwe, na elimu itolewe kuondoa mkanganyiko”, alisema



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, (wa pili kushoto) akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Kagera, Mhandisi Godlove Mathayo, (wa tatu kulia) wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wakulima nchini maarufu kama Nane Nane kwa Mkoa wa Kagera yaliofanyika katika Uwanja wa Kyakailabwa, wilayani Bukoba Mkoani humo, Agosti 8, 2021.

# Wakili Byabato - Waliobadilishiwa TARIFF watoe taarifa TANESCO zirekebishwe



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, (kushoto) na Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Bukoba wakiwa na moja ya mkungu wa ndizi, wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wakulima nchini maarufu kama Nane Nane kwa Mkoa wa Kagera yaliofanyika katika Uwanja wa Kyakailabwa, wilayani Bukoba Mkoani humo, Agosti 8, 2021.*

hususani wa Majumbaji , Wafabiashara, Viwanda Vidogo, Taa za Barabarani pamoja na Mabango, matumizi hayo ya umeme ni wastani wa zaidi ya Uniti 75 kwa miezi mitatu mfululizo.

Vilevile kwa kundi la Matumizi ya Juu ya Msongo(T2), wateja wa kundi hilo ni wale wenye matumizi ya kawaida ya wastani wa uniti 7500 kwa mwezi.

Na mwisho ni Kundi la Matumizi ya Juu ya Msongo wa Kati(T 3) ambapo wateja wake huunganishwa kwenye msongo wa kati wa umeme na matumizi yao

## Wakili Byabato.

Aidha alifafanua kuwa katika Kundi la Matumizi Madogo ya Nyumbani (D1), ambao linahusisha wateja wenye matumizi ya wastani wa Uniti 75 kwa mwezi watapaswa kulipa gharama ya shilingi 9150 na kwamba katika kundi hilo, mteja atatozwa bei ya juu zaidi kwa kila uniti itakayozidi 75 kwa mwezi.

Katika kundi la Matumizi ya Kawaida (T1), linahujumuisha wateja wenye matumizi ya kawaida ya umeme



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, (katikati) na wenyeji wake akiwasili katika Maadhimisho ya Siku ya Wakulima nchini maarufu kama Nane Nane kwa Mkoa wa Kagera yaliofanyika katika Uwanja wa Kyakailabwa, wilayani Bukoba Mkoani humo, Agosti 8, 2021.*

# Wakili Byabato - Waliobadilishiwa TARIFF watoe taarifa TANESCO zirekebishwe

ni zaidi ya Uniti 500 na umeme hupimwa kwa kilovolti 11 na zaidi.

Katika hatua nyingine aliwaeleza Wakazi wa Mkoa wa Kagera kuwa Wizara ya Nishati Kupitia TANESCO wataweka Umeme katika eneo la kibiasha la Mkoa lilipo katikati ya Wilaya ya Misenyi na Bukoba Vijijini ili eno hilo lianze kutumiwa na wafanyabisha pamoja na shughuli mbalimbali za

kiuchumi.

Kwa mantiki hiyo aliwataka wafanyabishara kuendelea kuwekeza zaidi vitega uchumi katika eneo hilo kwa kuwa kutakuwa na umeme wa uhakika.

Wakati huohuo aliwataka baadhi ya watumiaji wa TANESCO wasio waaminifu kuacha tabia ya kuomba rishwa kwa wateja ili waunganishiwe umeme

kwa kuwaambia kuwa wajiongeze akieleza kuwa kauli hiyo ni kitendo cha kuomba rushwa kwa wateja.

Hali kadhalika aliwaeleza wakazi wa Kagera kuwa hivi karibuni maeneo yote ambayo hayajafikiwa na umeme yatafikiwa kwa kuwa tayari wakandarasi wako kazini kutekeleza kazi hiyo kwa gharama ya shilingi 27,000 tu.

Na aliwasisitiza kuwa

endapo afisa yeyote kutoka TANESCO, au mkandarasi atataka kupewa chochote ili kumuunganishia umeme mwananchi, au akamtaka mwananchi ajiongeze ilia pate umeme, mwananchi huyo atoe taarifa sehemu husika, na ikiwezekana ampige picha na kurekodi kwa ushahidi zaidi kwa kwakuwa kufanya hivyo ni kuomba rushwa.



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wananchi waliofika kwenye Maadhimisho ya Siku ya Wakulima nchini maarufu kama Nane Nane kwa Mkoa wa Kagera yaliofanyika katika Uwanja wa Kyakailabwa, wilayani Bukoba Mkoani humo, Agosti 8, 2021.*

## Serikali kuingiza umeme wa Jotoardhi kwenye gridi ya Taifa

Na **Teresia Mhagama,**

**W**aziri wa Nishati, Dkt. Medard

Kalemani ameagiza kuharakishwa kwa utekelezaji wa miradi ya uzalishaji umeme wa Jotoardhi ili kuingiza megawati 40 katika gridi ya Taifa ifikapo mwakani.

Maagizo hayo aliyatoa wakati alipotembelea mradi wa nishati ya Jotoardhi wa Kiejo Mbaka ulioko wilayani Rungwe Mkoa wa Mbeya.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akifungua valvu ya kisima cha nishati ya Jotoardhi kinachotoa maji ya moto katika Mradi wa Kiejo Mbaka ulioko Wilaya ya Rungwe Mkoani Mbeya. Kushoto kwake ni Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi (TGDC), Mha. Kato Kabaka

“Tunataka kwenye gridi ya Taifa tuingize

umeme unaotokana na rasilimali ya Jotoardhi,

tuanze na megawati 30 za Mbozi (Songwe) na hizi megawati 10 (Kiejo Mbaka) tuwe na megawati 40 mwakani.” alisema Dkt Kalemani.

Alitaka wataalam kuongeza kasi ili mradi huo ukamilike mwezi Disemba mwaka 2022.

Aliongeza kuwa, katika gridi ya Taifa hakuna umeme wa nishati ya Jotoardhi ila kwa sasa jitihada zinafanywa na Serikali ili kuwa na umeme huo katika gridi ya taifa.

Dkt. Kalemani alimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kushoto) akifafanua jambo alipotembelea mradi wa jotoardhi wa Kiejo Mbaka ulioko Wilaya ya Rungwe Mkoani Mbeya, kulia ni Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi (TGDC), Mha. Kato Kabaka.

## Serikali kuingiza umeme wa Jotoardhi kwenye gridi ya Taifa

kutoa shilingi bilioni 1.15 katika utekelezaji wa mradi wa Kiejo Mbaka.

Katika hatua nyingine Dkt. Kalemani aliipongeza Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) kwa kutumia wataalam wa ndani katika utekelezaji wa mradi huo.

Aidha, aliagiza kuimarishwa kwa ulinzi katika eneo la mradi ili kuzuia watu wenye

nia mbaya kuhujumu miondombinu uliyopo kwenye eneo la mradi huo.

Kwa upande wake, Meneja Mkuu wa TGDC, Mha. Kato Kabaka alisema kuwa kwa sasa mradi huo upo katika hatua ya uhakiki wa rasilimali ya Jotoardhi iliyopo kwa kuchoronga visima katika eneo la mradi.

“Hatua hii ya

uchorongaji wa visima vifupi vitatu (3) vya utafiti, ina lengo la kuongeza taarifa za kisayansi ambazo zitatoa tathimini bora ya kuchoronga visima virefu vya uhakiki wa Jotoardhi,” alifafanua Mha. Kabaka

Aidha, alisema kuwa majimoto yaliyopatikana kutokana uchorongaji huo yanatarajiwa kutumika katika

matumizi kama vile kukausha mazao, kilimo cha nyumba vitalu, ufugaji na uchakataji wa bidhaa za viwandani.

Mha. Kabaka alisema “hatua hii itaisadia kuharakisha matumizi ya Jotoardhi katika shughuli za kiuchumi na kijamii, huku TGDC ikiongeza vyanzo vyake vya ndani vya mapato,”



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akigusa maji ya moto katika kisima cha nishati ya Jotoardhi katika mradi wa Kiejo Mbaka. Kulia ni Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi (TGDC), Mha. Kato Kabaka

## Dkt. Kalemani: Wakandarasi Marufuku kuhamisha nguzo zilizosimikwa, mnachonganisha Wananchi na Serikali

**Zuena Msuya,  
Ruvuma**

# W

akandarasi wanaotekeleza mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini katika maeneo yote nchini wametakiwa kuacha tabia ya kuhamisha nguzo za umeme zilizosimikwa kwakuwa kufanya hivyo ni kuchonganisha Serikali na Wananchi wake.

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani alieleza hayo wakati akizindua Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, katika Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma, Agosti 02, 2021.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na Wakazi wa Kijiji cha Matiri (hawapo pichani) wakati akizindua Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, katika Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma, Agosti 02, 2021.

Mzunguko wa Pili, katika Kijiji cha Matiri wilayani Mbinga mkoani Ruvuma, Agosti 02, 2021.

Dkt. Kalemani alieleza kuwa, mkandarasi yeyote aliyesimika nguzo, haruhusiwi kuondoa nguzo hizo na kupeleka

sehemu nyingine badala yake ahakikishe anasambaza umeme katika eneo hilo na kuunga wateja wa eneo hilo, na atafute nguzo zingine za kupeleka eneo alilokusudia na kutekeleza mradi.

“Sitaki kuona mkandarasi anafikisha nguzo ‘Site’ anazisimika, au mwingine amezirundika hapo baada ya muda anazitoa wakati hapo na hakuna umeme anapeleka sehemu nyingine ni marufuku!, huku ni kugombanisha Serikali na Wananchi wake, Wananchi wanafahamu serikali imetoa fedha nyingi kuhakisha vijiji vyote vinapata umeme bila kurukwa, unapohamisha nguzo hizo unapeleka ujumbe gani kwa wananchi!” alisema Dkt. Kalemani.

Akizungumzia Usambazaji wa Umeme katika Wilaya ya Mbinga, Dkt. Kalemani alisema



Maafisa kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakichukua taarifa ya Mkazi wa Kijiji cha Matiri, Christopher Ngonyani (katikati) baada ya kukabidhiwa kifaa cha Umeme Tayari (UMETA) na Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani wakati akizindua Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, wilayani Mbinga mkoani Ruvuma, Agosti 02, 2021.



Maafika kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakipata maelekezo kutoka kwa Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) wakati wa uzinduzi wa Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, wilayani Mbinga mkoani Ruvuma, Agosti 02, 2021.



## Dkt. Kalemani: Wakandarasi Marufuku kuhamisha nguzo zilizosimikwa, mnachonganisha Wananchi na Serikali



Baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Matiri wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) wakati akizindua Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, wilayani Mbinga mkoani Ruvuma, Agosti 02, 2021.

kukamilisha mradi huo ndani ya muda uliopangwa kwa mujibu wa mkataba, na kwamba 10% ya malipo yake yatakwa kwa kuchelewesha kazi husika.

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya Vijiji 554 ambapo vijiji 289 tayari vinaumeme na 265 bado havijafikiwa katika Wilaya za Songea, Mbinga, Nyasa, Tunduru na Mamtumbo kwa gharama za Bilioni 71.95 kwa mkoa mzima.

kuwa wilaya hiyo inajumla ya Vijiji 169, kati ya hivyo 71 vimepatiwa umeme na 98 vitapatiwa umeme katika mradi huo wa REA III mzunguko wa pili kwa gharama ya shilingi Bilioni 14.34.

Hata hivyo aliwaagiza wakandarasi wanaotekeleza mradi huo Kampuni ya NAMIS kuanza kusambaza umeme katika Kijiji cha Matiri kuanzia mwezi huu (Agosti), 2021.

Aliwasisitiza wakandarasi hao kuwa serikali haitaongeza muda kwa mkandarasi yeyote atakayechelewa



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akikata utepe katika Shule ya Msingi Ilaya wakati akizindua Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, wilayani Mbinga mkoani Ruvuma, Agosti 02, 2021.

# Alama zinazoonekana ziwekwe katika eneo la mradi wa LNG-Dkt.Kalemani

**Na Teresia  
Mhagama, Lindi**

**W**aziri wa Nishati, Dkt. Medard

Kalemani, ameliagiza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuweka alama zinazoonekana kuzunguka eneo la mradi wa Kuchakata na kusindika Gesi Asilia (LNG) katika eneo la Likong'o wilayani Lindi, Mkoa wa Lindi.

Dkt.Kalemani alitoa agizo hilo baada ya kutembelea eneo hilo akiwa ameambatana na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuberi, baadhi ya Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na wawekezaji wa mradi huo, kampuni ya Equinor na Shell.

“ Eneo tumeligharamia hivyo ni muhimu likawekwa alama zinazoonekana



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizungumza wakati wa mkutano wa Waziri wa Nishati na Wadau wa Maendeleo Mkoa wa Lindi uliofanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi. Kulia kwake ni Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani na kushoto kwake ni Mbunge wa Mchinga, Salma Kikwete.*

badala ya kuweka

bango pekee ili eneo hili liweze kutambulika na wananchi wasije kulivamia au kutumika vibaya, hivyo tuna wajibu wa kulinda eneo hili na kuonesha kuwa kuna kazi inakuja.” Alisema Dkt.Kalemani

Aidha, Dkt. Kalemani alitoa agizo kwa TPDC, ndani ya siku Tano wawe wamekamilisha taratibu za upatikanaji wa mkandarasi kutoka mkoani Lindi atakayeweka alama hizo za mipaka na mkandarasi huyo aanze kazi mara moja.

Aidha, alitoa agizo kwa TPDC kuhakikisha kuwa, eneo hilo lenye ukubwa wa hekta



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akizungumza wakati wa mkutano wake na Wadau wa Maendeleo mkoani Lindi uliohusu mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (LNG). Kushoto kwake ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato na kulia kwake ni Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga.*

## Alama zinazoonekana ziwekwe katika eneo la mradi wa LNG-Dkt.Kalemani



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akiangalia alama iliyowekwa katika eneo la mradi wa kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (LNG) katika eneo la Likong'o wilayani Lindi, Mkoa wa Lindi. Pamoja naye ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kushoto kwa Waziri), Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga (kulia kwa Waziri). Wengine katika picha ni Kamishna wa Petrol na Gesi, Adam Zuberi, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio na watendaji wengine kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara.

2,071 linasafishwa na kuwaasa wananchi kutovamia eneo hilo kwani limeshatwaliwa na Serikali baada ya wananchi hao kulipwa fidia.

Kabla ya kutembelea eneo hilo, viongozi hao walikutana na wadau wa maendeleo Mkoa wa Lindi pamoja na baadhi ya Wabunge wa Mkoa wa Lindi ambao ni Mbunge wa Mchinga, Salma Kikwete na Mbunge wa Lindi Mjini, Hamida Abdallah ili kueleza

hatua mbalimbali za utekelezaji wa mradi huo.

Dkt. Kalemani aliwaeleza wadau hao kuwa, Serikali imetoa takriban shilingi bilioni 5.72 kwa ajili ya kulipa fidia wananchi wa eneo hilo kazi ambayo ilikamilika mwaka jana.

Alisema kuwa, mwezi Mei mwaka huu majadiliano yameanza na wawekezaji kuhusu utekelezaji wa mradi huo na yanatarajiwa kufikia mwisho mwezi Oktoba mwaka huu.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, alisema kuwa Serikali itaendelea kuwahamasisha wananchi mkoani Lindi kuwa mstari wa mbele katika shughuli za kujiletea maendeleo kutokana na uwepo wa nishati kama vile umeme na Gesi.

Alisema kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita imetoa fedha za kutosha ili kufikisha huduma ya umeme na nishati nyingine kwa wananchi na Wizara ya Nishati ipo tayari kwa ajili ya kuwahudumia wananchi hao.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Adolf Ndunguru pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali pamoja na watendaji kutoka Wizara hizo pamoja na TANESCO wakiwa katika chumba cha kuendesha mitambo ya umeme ya Kinyerezi II inayozalisha umeme wa megawati 240 mkoani Dar es Saalam.

## Bilioni 71.9 kutekeleza REA III Mzunguko wa Pili Ruvuma, mradi wazinduliwa Tunduru

### Na Zuena Msuya, Ruvuma

meelezwa kuwa shilingi Bilioni 71.95 zitatumika kutekeleza mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu (REA III), Mzunguko wa Pili katika vijiji vyote ambavyo havijapekelewa umeme mkoani Ruvuma.

Hayo yameelezwa na Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani wakati akizindua mradi huo kwa Mkoa wa Ruvuma, ambapo uzinduzi huo ulifanyika katika Kijiji cha Nalasi wilayani Tunduru



Waziri wa Nishati, Dkt, Medard Kalemani (kushoto) akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Nalasi wilayani Tunduru mkoani Ruvuma wakati akizindua mradi wa usambazaji umeme Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili kwa mkoa huo uliofanyika wilyani humo, Agosti 01, 2021.

mkoani humo Agosti 01, 2021.

Dkt. Kalemani alisema kuwa fedha hizo zitatumika kufikisha na kusambaza umeme katika Vijiji 265 vilivyobakia katika mkoa

huo wenye jumla ya vijiji 554, ambapo tayari vijiji 289 vimeshafikiwa na umeme.

“Wanaruvuma hasa Tunduru tulipozindua mradi huu hakikisheni mnautumia umeme

huu ipasavyo kwa kujiletea maendeleo pia anzisheni viwanda, Rais wa awamu ya Sita, Samia Suluhu Hasan ametoa fedha za kutosha kuhakikisha vijijini vyote vinapata



Baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Nalasi wilayani Tunduru mkoani Ruvuma wakifurahia jambo, wakati Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) akizungumza kabla ya kuzindua Mradi wa usambazaji Umeme Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili kwa Mkoa huo uliofanyika wilayani humo, Agosti 01, 2021.



Baadhi wa Vijana wa Kijiji cha Nalasi wilayani Tunduru mkoani Ruvuma wakimsikiliza waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) wakati akizindua Mradi wa usambazaji Umeme Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili kwa mkoa wa Ruvuma uliofanyika wilayani humo, Agosti 01, 2021.

## Bilioni 71.9 kutekeleza REA III Mzunguko wa Pili Ruvuma, mradi wazinduliwa Tunduru



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Balozi Brigedia Generali Wilbert Ibuge (kulia) akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Nalasi wilayani Tunduru mkoani Ruvuma wakati wa uzinduzi wa Mradi wa usambazaji Umeme Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili kwa mkoa wa Ruvuma uliofanyika wilayani humo, Agosti 01, 2021.

Waziri wa Nishati, Dkt, Medard Kalemani (tatu kushoto) akiweka Jiwe la Msingi katika Kijiji cha Nalasi wilayani Tunduru mkoani Ruvuma wakati akizindua Mradi wa usambazaji Umeme Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili kwa Mkoa huo, uliofanyika wilayani humo, Agosti 01, 2021.

umeme ifikapo Desemba 2022, sasa kazi kwenu kuandaa nyumba zenu na kwa sasa umeme ni lazima sababu Serikali imegharamia kila kitu, ninyi mtalipia shilingi 27,000 tu, hivyo msichezee nafasi hii, pia ni marufuku kununua nguzo" alisema Dkt. Kalemani.

Alifafanua kuwa kampuni mbili za kitanzania zimepewa dhamana ya kutekeleza mradi huo katika wilaya zote za mkoa husika ambazo ni Songea, Mbinga, Tunduru, Nyasa na Namtumbo, ambapo kazi hiyo imegawanywa

katika makundi mawili.

Wakandarasi hao ni Kampuni ya NAMIS itayotekeleza mradi huo katika Wilaya za Songea, Mbinga na Nyasa kwa gharama ya TZS. Bilioni 35.281, na White City itatekeleza katika Wilaya za Tunduru na Namtumbo kwa gharama ya Bilioni 36.678.

Akizungumzia wilaya ya Tunduru ambapo ndipo mradi huo umezinduliwa kimkoa, Dkt. Kalemani alisema kuwa wilaya hiyo ina jumla ya vijiji 157, kati ya hivyo vijiji vyenye umeme ni 72 na visivyo na umeme ni 85.

Vijiji hivyo 85 vilivyosalia vitapelekewa umeme kupitia mradi huo uliozindiwa kwa gharama ya shilingi Bilioni 21.7 ambapo utatekelezwa kwa kipindi cha miezi 12.

Kwa wilaya hiyo ya umeme utaanza kupelekwa katika kata ya Nalasi ikihusisa vijiji, vitongoji na mitaa vyote vya kata hiyo.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Balozi Brigedia Generali Wilbert Ibuge aliwataka wakazi wa mkoa huo kuwa walinzi wa miundombinu ya umeme pamoja na kutoa ushirikiano

kwa wakandarasi watakaotekeleza mradi huo.

Balozi Ibuge aliwataka vijana wa maeneo husika kuchangamkia fursa ya kufanya kazi zisizo na taaluma maalum, ili kuweza kujipatia kipato na kunufaika na mradi huo.

Hata hivyo aliwataka wakandasi waliopewa dhamana ya kutekeleza mradi huo kujitambulisha katika ofisi za serikali za mitaa, wakati wa kutekeleza miradi hiyo ili kupata ushirikiano zaidi na kurahisisha utendaji kazi wao.

# Mradi wa Umeme wa Ujazilizi Mkoa Kilimanjaro wazinduliwa Same

**Mkandarasi NJARITA na OCTOPUS kukatwa 10% kwa kuchelewesha Mradi**

**Na Zuena Msuya,  
Kilimanjaro**

**W**aziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani amezindua Mradi wa umeme wa Ujazilizi Fungu la Pili kwa Mkoa wa Kilimanjaro na kuagiza kukatwa 10% ya malipo ya wakandarasi Kampuni ya NJARITA

na OCTOPUS kwa kutokamilisha Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili (REA II) mkoani humo. Aidha ameiagiza Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Same, kumsaka na kumuweka ndani mkandarasi NJARITA kwa kutokuwepo eneo la mradi. Dkt.Kalemani alitoa agizo hilo wakati



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani(Kulia) akizungumza na Mmoja wa wanafunzi wa shule ya msingi Kalemani wakati wa uzinduzi wa Mradi wa umeme wa Ujazilizi Fungu la Pili kwa Mkoa wa Kilimanjaro uliofanyika wilayani Same, Julai 29, 2021.

akizindua Mradi wa umeme wa Ujazilizi Fungu la Pili kwa Mkoa Kilimanjaro uliofanyika wilayani Same kwa

kuwasha umeme katika Kijiji cha Muheza Kata ya Maore, Nasuro Kata ya Mwembe wilayani humo, Julai 29, 2021.

Aidha aliwawashia umeme wateja waliounganishwa kupitia mradi huo katika Kijiji cha Kifarū wilayani Mwanga, Kijiji cha Nganjoni Wilaya ya Moshi na Kijiji cha Nkweseko Kitongoji cha Kyareni katika Wilaya ya Hai mkoani humo.

Akizungumzia kukatwa 10% ya malipo ya wakandarasi, Dkt. Kalemani alisema kuwa wakandarasi hao NJARITA na OCTOPUS, walipewa jukumu la kutekeleza Mradi wa REA II katika mkoa



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani(Kulia) akizungumza na Mmoja wa wanafunzi wa shule ya msingi Kalemani wakati wa uzinduzi wa Mradi wa umeme wa Ujazilizi Fungu la Pili kwa Mkoa wa Kilimanjaro uliofanyika wilayani Same, Julai 29, 2021.

# Mradi wa Umeme wa Ujazilizi Mkoa Kilimanjaro wazinduliwa Same



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (Katikati) akizungumza na Mkuu wa Wilaya ya Mwanza, Abdallah Mwaipaya (wa tatu kulia) kabla ya kukata utepe kuwasha umeme katika Kijiji cha Kifaru wakati wa ziara ya uzinduzi wa Mradi wa umeme wa Ujazilizi Fungu la Pili kwa Mkoa wa Kilimanjaro uliofanyika wilayani Same, Julai 29, 2021.

huo wa Kilimanjaro kwa Makubaliano ya mkataba wa utekelezaji wa mradi huo kwa kipindi cha miezi 24 kuanzia mwaka 2013.

Dkt. Kalemani alisema kuwa wakandarasi hao hawakukamilisha kazi hiyo kwa wakati ulipangwa na walieleza changamoto mbalimbali walizokutana nazo katika kutekeleza mradi huo, na kulazimika kuongezwa muda wa kufanya kazi hiyo, hata hivyo baada ya kuongezwa muda hawakuweza kukamilisha mradi huo kwa wakati.

“Mkuu wa Wilaya

na Kamati ya Ulinzi mtafuteni mkandarasi

Njalita na awekwe korokoroni kwa sababu hayupo eneo la mradi, pia nawaagiza REA, kukata 10% ya malipo ya kazi yaliyosalia kwa kazi iliyofanywa na wakandarasi NJARITA na OCTOPUS kwa kuwa mpaka sasa hawajakamilisha kazi waliopewa, wakati taratibu zingine za kisheria zikiendelea kufanyika, hatuwezi kuvumilia tena vitu kama hivi wakati malipo yalikuwa yakifanyika kwa wakati!”, alisema

Dkt. Kalemani.

Kuhusu Mradi wa Ujazilizi fungu la Pili, Dkt. Kalemani alisema kuwa, utakamilisha usambazaji wa umeme katika vijiji vyote vilivyobaki katika mkoa huo pamoja na kuwawashia umeme wateja waliolipia.

Aliwafafanulia wananchi wa mkoa huo kuwa, mradi huo wa ujazilizi utatekelezwa ndani ya kipindi cha miezi 12 kwa kuwafikiwa wateja wote kwa nyakati tofauti.



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (wa tatu kulia) akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Nganjoni Wilaya ya Moshi wakati wa ziara ya uzinduzi wa Mradi wa umeme wa Ujazilizi Fungu la Pili kwa Mkoa wa Kilimanjaro uliofanyika wilayani Same, Julai 29, 2021.

# Mradi wa Umeme wa Ujazilizi Mkoa Kilimanjaro wazinduliwa Same

Kufuatia mradi huo aliwataka wakazi wa maeneo ambayo bado hayajafikiwa na umeme watayarishie nyumba zao kwa kutandaza nyaya pamoja na kulipia ili kufungiwa umeme kwa gharama ya shilingi 27,000 tu.

Kampuni ya Kitanzania ya Derm imepewa dhamana ya kutekeleza mradi wa uzajilizi katika maeno yote yaliyobaki katika

Mkoa wa Kilimanjaro ambapo pamoja na mambo mengine tayari amewasha umeme katika baadhi ya vijiji vya Wilaya ya Same, Mwanga, na Hai huku kazi ikiendelea.

Aidha mkandarasi huyo ametakiwa kutumia vijana waliopo katika maeneo yanayozunguka mradi kufanya kazi zile zisizo na taaluma maalum ili kila moja ajivunie na

kufurahia uwepo mradi huo.

Sambasamba na hilo, wakazi wa mkoa huo wametakiwa kuwa walinzi wa vifaa na miundombinu umeme vitakavyotumika katika kutekeleza mradi huo ili kurahisisha utekelezaji huo na kukamilika kwa haraka na kwa wakati uliopangwa pia ushirikiano kwa mkandarai huo.

Mkoa wa Kilimanjaro

kwa sasa una jumla ya Megawati 137 za umeme, matumizi halisi ni Megawati 41 tu, hivyo wakazi wa mkoa huo wametakiwa kuchamkia fursa mradi huo kuweza kutumia umeme wote uliopo katika mkoa huo kwa kufanya shughuli mbalimbali za kujiletea maendeleo na taifa kwa ujumla.



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani, (Katikati) akizungumza na Wakazi wa Kijiji cha Nkweseko Kitongoji cha Kyareni (hawapo pichani) wilayani Hai wakati wa ziara ya uzinduzi wa Mradi wa umeme wa Ujazilizi Fungu la Pili kwa Mkoa wa Kilimanjaro uliofanyika wilayani Same, Julai 29, 2021.



# KAZI YA KULETA UMEME VIJIJINI INAENDELEA – NAIBU WAZIRI BYABATO

**Veronica Simba na  
Hafsa Omar – Pwani**

**N**aibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato amesema kuwa kazi ya kusambaza umeme vijijini inaendelea kutekelezwa kwa ufanisi nchini kote kupitia miradi mbalimbali.

Aliyasema hayo wakati akizindua Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili Mkoa wa Pwani, katika Hafla iliyofanyika kijiji cha Mikere, Kata ya Njia Nne, wilayani Mkuranga

Agosti 26 mwaka huu.

Akizungumza na wananchi wakati wa Hafla hiyo, Naibu Waziri alieleza kuwa uzinduzi huo ni mojawapo ya mafanikio makubwa ya Serikali kwani unakamilisha ngwe ya mwisho ya upelekaji umeme katika vijiji vilivyosalia.

Alibainisha kuwa Serikali imetenga shilingi bilioni 37.431 kwa ajili ya kuvifikishia umeme vijiji vyote 89 vilivyosalia katika Mkoa wa Pwani.

Kwa upande wa Wilaya ya Mkuranga, Naibu Waziri alibainisha kuwa jumla ya shilingi bilioni 16.823



Naibu Waziri wa Nishati Stephen Byabato (katikati), akipiga makofi baada ya kuwasha rasmi umeme katika Ofisi ya Kijiji cha Mikere, Kata ya Njia Nne, wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani. Naibu Waziri aliwasha umeme huo ikiwa ni uzinduzi rasmi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Pwani Agosti 26, 2021. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya hiyo Hadija Nasri na kulia ni Mbunge wa Jimbo la Mkuranga ambaye pia ni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega.

zimetengwa kwa ajili ya kuvifikishia umeme vijiji



Naibu Waziri wa Nishati Stephen Byabato akizungumza na wananchi wa kijiji cha Mikere, Kata ya Njia Nne, wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani, wakati wa Hafla ya uzinduzi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, Ngazi ya Mkoa, Agosti 26, 2021.



Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Romanus Lwena akiwasilisha taarifa kuhusu Wakala huo, wakati wa hafla ya uzinduzi rasmi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, Mkoa wa Pwani, uliofanyika katika kijiji cha Mikere, Kata ya Njia Nne, wilayani Mkuranga, Agosti 26 mwaka huu.

# KAZI YA KULETA UMEME VIJIJINI INAENDELEA – NAIBU WAZIRI BYABATO



Naibu Waziri wa Nishati Stephen Byabato (wa pili-kushoto) akishirikiana na viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Pwani, kukata utepe ili kuzindua rasmi Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, Mkoa wa Pwani. Tukio hilo lilifanyika katika kijiji cha Mikere, wilayani Mkuranga Agosti 26, 2021. Wa kwanza kushoto ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Hadija Nasri na kushoto kwa Naibu Waziri ni Mbunge wa Mkuranga ambaye pia ni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega.

vyote 40 vilivyosalia.

Aidha, Naibu Waziri aliwahasisha wananchi kutumia fursa hiyo adhimu ya umeme kuboresha maisha yao kwa kuutumia kwenye miradi ya uzalishaji mali pamoja na huduma mbalimbali za kijamii.

“Tunawahimiza wananchi kuanzisha viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na madini pamoja na kuboresha utoaji huduma za afya, elimu, maji, mawasiliano na nyinginezo,” alisisitiza.

Naye Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Romanus Lwena alibainisha kuwa, Awamu hiyo ya Tatu ya Mradi, Mzunguko wa Pili itatekelezwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

“Mradi huu umelenga kufikisha huduma ya umeme kwenye vijiji na vitongoji 3,448 na utanufaisha wateja wa awali 75,622 kwa kipindi cha miezi 18 na gharama ya shilingi trilioni 1.3,” alifafanua.

Akitoa salamu za ukaribisho, Mbunge wa Jimbo la Mkuranga ambaye pia ni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega aliipongeza Serikali kwa

utekelezaji mzuri wa miradi ya maendeleo kwa wananchi ikiwemo miradi ya umeme vijijini.

Ulega aliiomba Serikali kupitia Wizara ya Nishati na REA, kukamilisha ahadi ya kuvipelekea umeme vijiji vilivyosalia ili wakazi wake nao wanufaike na nishati hiyo muhimu.

Mradi wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili mkoani Pwani, unatekelezwa na Mkandarasi China Railway Construction Electrification Bureau Group Company Ltd (CRCEBG) na umefadhiliwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia.



Wananchi wa Kijiji cha Mikere, Kata ya Njia Nne, wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani, wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati Stephen Byabato (hayupo pichani) alipokuwa akizungumza nao wakati wa hafla ya uzinduzi rasmi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, Ngazi ya Mkoa, uliofanyika katika kijiji hicho, Agosti 26, 2021.

# EREA yajitambulisha kwa Dkt. Kalemani

**Zuena Msuya,  
Dodoma,**

**W**aziri wa Nishati, Dkt. Medard

Kalemani ameahidi kufanya kazi kwa ushirikiano na Muungano wa Taasisi za Udhhibiti wa huduma za Mafuta na Umeme kwa nchi sita (6) za Afrika Mashariki (EREA) mara tu taasisi hiyo itakapokamilisha



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kushoto) akizungumza na Katibu Mtendaji wa Muungano wa Taasisi za Udhhibiti wa huduma za Mafuta na Umeme kwa nchi sita (6) za Afrika Mashariki (EREA), Dkt. Geoffrey Mabea, (kulia) alipofika ofisini kwa waziri huyo Jijini Dodoma, Agosti 17, 2021, kutambulisha taasisi hiyo.



Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu Wizara ya Nishati, Edward Ishengoma (kushoto), Kamishna wa Mafuta na Gesi, Adam Zuberi (kulia), Mhandisi Shkurani Rugaimukamu Wizara ya Nishati (pili kushoto) na Mhasibu Mkuu wa (EREA) Augustino Massawe wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) wakati akizungumza na ujumbe wa Muungano wa Taasisi za Udhhibiti wa Huduma za Mafuta na Umeme kwa nchi sita (6) za Afrika Mashariki (EREA).

taratibu zinazotakiwa.

Dkt. Kalemani alisema hayo wakati wa mazungumzo na Katibu Mtendaji wa EREA, Dkt. Geoffrey Mabea na ujumbe wake, walipofika ofisini kwa Waziri huyo jijini Dodoma, Agosti 17, 2021, kujitambulisha, kwa lengo la kueleza majukumu yao juu ya muungano huo na namna inavyofanya kazi kwa nchi husika.

Dkt. Kalemani alisema kuwa Wizara ya Nishati, iko tayari kushirikiana na EREA katika kutekeleza majukumu yake kwa manufaa ya nchi za Afrika Mashariki, kwakuwa

## EREA yajitambulisha kwa Dkt. Kalemani



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kushoto) akimsikiliza Katibu Mtendaji wa Muungano wa Taasisi za Udhhibiti wa huduma za Mafuta na Umeme kwa nchi sita (6) za Afrika Mashariki (EREA), Dkt. Geoffrey Mabea (wa pili kulia) alupofika ofisini kwa waziri kutambulisha taasisi hiyo, wa pili kulia ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya usimamizi wa huduma za Nishati na Maji (EWURA), Mhandisi Godfrey Chibulunje.

nchi hizo zimekuwa zikishirikiana katika mambo mbalimbali ya kimaendeleo.

Aidha aliitaka taasisi hiyo kukamilisha rasimu ya Mkataba wa utekelezaji wa majukumu yake ili isambazwe kwa nchi husika ili kila moja iweze kutoa maoni yake.

Sambasamba hilo alizishukuru taasisi za kifedha hasa Benki ya Dunia (WB) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa kufadhili wa uundwaji wa Taasisi hiyo na kuwa bega kwa beka katika kukuza Sekta ya

Nishati nchini.

Kwa upande wake, Katibu Mtendaji wa EREA, Dkt. Geoffrey Mabea, aliipongeza Tanzania kupitia Wizara ya Nishati kwa kuwa nchi ya tatu (3) Afrika katika uthibiti wa masuala ya nishati.

Vilevile alieleza kuwa taasisi hiyo ina malengo makubwa matatu, moja likiwa ni kuwezesha muunganiko wa kisera katika masuala ya nishati kwa nchi wanachama katika kazi za udhibiti wa bei za mafuta na umeme.

Pia kufanya tafiti

za kisera hususani katika sekta ya nishati na kuwezesha ushirikishwaji wa taarifa kwa nchi za Afrika Mashariki na kujenga uwezo kwa Taasisi za Udhhibiti kwa nchi wanachama pamoja na washirika wote katika sekta ya nishati.

Dkt. Mabea alitaja nchi wanachama katika taasisi hiyo kuwa ni Tanzania, Kenya, Rwanda, Burundi, Uganda na Sudani Kusini ambapo makao makuu ya tasisi hiyo yapo mjini Arusha, na kwamba ilianzishwa

rasmi mwaka 2009.

Hata hivyo alieleza kuwa, tayari imeandaliwa rasimu ya Mkataba wa Makubaliano ambao utasambazwa kwa nchi wanachama ili waweze kutoa maoni, na Mkataba huo ukikamilika utapelekwa kwa kila nchi wanachama ili uweze kusainiwa.

Lengo la mkataba huo ni kusaidia kuridhia ujenzi wa Chuo cha Udhhibiti kinachotarajiwa kujengwa Nchini Tanzania katika Jiji la Arusha.

# Tathmini ya upelekaji umeme mijini kwa sh.27,000 kufanyika ndani ya miezi mitatu

**Na Teresa Mhagama, Songwe**

**W**aziri wa Nishati, Dkt. Medard

Kalemani, amesema kuwa tathmini ya agizo la Serikali la kupeleka umeme mijini na vijijini kwa shilingi 27,000 itafanyika ndani ya miezi mitatu ili kuona kama agizo hilo linatekelezwa ipasavyo.

Waziri wa Nishati alisema hayo tarehe 27 Agosti, 2021 wilayani Mbozi, Mkoa wa Songwe wakati akizungumza na Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, Cosmas Ishenye, Mkuu



*Meneja wa TANESCO, Mkoa wa Songwe, Grace Mtungi (wa kwanza kushoto) akitoa maelezo kwa Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (wa Pili kutoka kulia) kuhusu mitambo iliyopo katika kidogo cha kupoza umeme wilayani Mbozi, Mkoa wa Songwe. Wa kwanza kulia ni Mbunge wa Mbozi, George Mwenisongole. Kulia kwa Waziri ni Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, Cosmas Ishenye. Wengine ni wataalam kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).*

wa Wilaya ya Ileje, Anna Gidarya na Mbunge wa Mbozi, George Mwenisongole kabla ya kuzindua kimkoa mradi wa usambazaji umeme vijijini wa Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili.

“Suala la kupelekewa umeme kwa zaidi ya shilingi 27,000 halipo, pia suala la mwananchi kuuziwa nguzo halipo, mtu awe

tajiri au maskini bei ni moja tu ambayo ni shilingi 27,000 tu hivyo tutafuatilia kuona kama agizo hili linafanyiwa kazi na watendaji wetu.”

Alisema Dkt. Kalemani Alisema Serikali inataka wananchi wengi waunganishiwe umeme ili wautumie kwa shughuli mbalimbali hivyo aliwaagiza watendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kuongeza kasi ya kusambaza umeme na kuacha kuweka vikwazo vya kumpeleka mwananchi umeme kama vile malipo ya



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wananchi katika kijiji cha Bara, wilayani Mbozi, Mkoa wa Songwe, kabla ya kuzindua mradi wa usambazaji umeme vijijini wa Awamu ya Tatu, mzunguko wa Pili.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (wa Nne kutoka kulia) pamoja na viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Songwe wakikata utepe kuashiria uzinduzi wa mradi wa usambazaji umeme vijijini wa Awamu ya Tatu, mzunguko wa Pili katika mkoa huo. Kulia kwa Waziri ni Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, Cosmas Ishenye, Mbunge wa Mbozi, George Mwenisongole na Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Anna Gidarya.

# Tathmini ya upelekaji umeme mijini kwa sh.27,000 kufanyika ndani ya miezi mitatu



Mbunge wa Mbozi, George Mwenisongole (kulia) akizungumza na wananchi (hawapo pichani) katika Kijiji cha Bara, wilayani Mbozi wakati wa hafla ya kuzindua mradi wa usambazaji umeme vijijini wa Awamu ya Tatu, mzunguko wa Pili.

nguzo.

Akizungumzia hali ya upatikanaji umeme kwa Mkoa wa Songwe alisema kuwa, kwa sasa Mkoa huo umejengewa kituo kidogo cha kupoza umeme wakati Serikali ikifanya jitihada nyingine za kupeleka umeme wa uhakika mkoani humo.

Aliongeza kuwa, kuna mradi mkubwa wa kusafirisha umeme wa kV 400 kutoka Iringa, kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga ambao utaimarisha zaidi hali ya upatikanaji wa umeme katika mikoa hiyo pamoja na Songwe ambapo mkandarasi anatarajiwa kuanza kazi mwezi Februari

mwakani.

Akiwa wilayani Mbozi, Waziri wa Nishati alikagua kituo kidogo cha kupoza umeme wilayani humo na kuiagiza TANESCO kuanza kupeleka umeme kwa wananchi wanaozunguka eneo hilo ndani ya siku Kumi baada ya wananchi hao kulalamika kuwa hawana umeme.

Awali, Meneja wa TANESCO Mkoa wa Songwe, Grace Mtungi alisema kuwa mahitaji ya juu ya umeme mkoani humo ni megawati 13.5 huku uwezo wa mitambo ya umeme ukiwa ni megawati 15 hivyo Mkoa huo unapata

umeme wa kutosha mahitaji kwa sasa.

Aliongeza kuwa, idadi wa wateja waliounganishwa na umeme inaendelea kuongezeka kwani katika mwaka 2019/2020 wateja waliounganishwa umeme walikuwa ni 51,176 na kwa sasa kuna wateja 58,587.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Nishati alizindua Mradi wa usambazaji umeme vijijini wa Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Songwe ambao unatarajiwa kusambaza umeme katika Vijiji 127 kwa

gharama ya shilingi bilioni 42.3.

Katika uzinduzi huo, Waziri wa Nishati aliitaka kampuni ya Derm Electrics kufanya kazi ya usambazaji umeme mkoani humo kwa muda wa miezi 18 kwa kutumia vifaa vinavyopatikana nchini.

Kuhusu hali ya usambazaji umeme vijijini nchini, alisema kuwa, mpaka sasa takriban vijiji 10,312 vimeshasambaziwa umeme na vimebaki vijiji 1956 huku lengo likiwa ni Vijiji vyote kuwa na umeme ifikapo Disemba mwakani.



Chifu Mloto wa Msangawale, kiongozi wa jadi kutoka Tarafa ya Itaka wilayani Mbozi (kushoto) akimvalisha mgolole wenye bendera ya Taifa, Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani kutambua mchango wake katika kusimamia miradi ya usambazaji umeme.

## Mtambo wa kisasa wa kukausha nguzo za umeme wazinduliwa wilayani Mufindi

**M**tambo wa kwanza wa kisasa wa kukausha nguzo katika nchi za Afrika Mashariki na Kati umezinduliwa na Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani wilayani Mufindi Mkoa wa Iringa.

Hafla ya kuzindua mtambo huo ilifanyika katika kiwanda cha nguzo cha Sao Hill kilichopo wilayani Mufindi tarehe 29 Agosti, 2021 na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali

wa Mkoa wa Iringa wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Mufindi Saad Mtambule na Mbunge wa Mafinga, Cosato Chumi.

Akitoa taarifa kuhusu mtambo huo, Mwenyekiti wa Bodi ya Sao Hill, Godlisten Minja alisema kuwa maamuzi ya kufunga mtambo kwenye kiwanda hicho yamefanyika ili kuongeza ubora wa nguzo na kuongeza uzalishaji.

Alisema kuwa kwa kutumia mtambo huo



Nguzo za umeme zikiwa katika mtambo wa kisasa wa kukausha nguzo katika kiwanda cha Sao Hill kilichopo wilayani Mufindi Mkoa wa Iringa.

nguzo zinakaushwa kati ya siku nne hadi 12 kutegemea hali ya ubichi tofauti na kutumia jua kukausha nguzo

hizo ambapo nguzo hukaushwa kwa takriban miezi mitatu hadi minne.

Aliongeza kuwa mtambo huo una uwezo wa kukausha nguzo 800 hadi 900 kwa wakati mmoja kutegemeana na ukubwa wa nguzo.

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani aliipongeza Sao Hill kwa kufunga mtambo huo wa kisasa ambao haukuwepo hapa nchini na kufanya upanuzi wa uzalishaji wa nguzo katika kiwanda hicho.

Aliwahakikishia wazalishaji hao na wengine uhakika wa soko la nguzo hizo kwani kazi ya usambazaji umeme mijini na vijijini inaendelea. Aliwataka pia kuongeza uzalishaji wa



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (wa Tano kutoka kulia) akikata utepe kuzindua mtambo wa kisasa wa kukausha nguzo katika kiwanda kinachozalisha nguzo za umeme cha Sao Hill wilayani Mufindi Mkoa wa Iringa. Pamoja naye ni Mkuu wa Wilaya ya Mufindi Saad Mtambule (wa Tano kushoto), Mbunge wa Mafinga, Cosato Chumi (wa Tatu kulia), Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya Sao Hill George Botther (wa Pili kulia), Mwenyekiti wa Bodi ya Sao Hill Godlisten Minja (wa Nne kulia). Wengine katika picha ni watendaji kutoka TANESCO na Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

# Mtambo wa kisasa wa kukausha nguzo za umeme wazinduliwa wilayani Mufindi



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ( wa Pili kulia), akiwa katika gari la kampuni ya kuzalisha nguzo ya Qwihaya ambalo limepakia nguzo tayari kwa kuzipeleka Itigi, wilayani Manyoni kwa ajili ya kazi ya usambazaji umeme vijijini. Pamoja naye ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe, Judica Omari ( Wa pili kushoto), Mkuu wa Wilaya Ludewa, Tsere Andrea ( Wa tatu kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Qwihaya, Leonard Mahenda ( wa kwanza kushoto).



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ( wa kwanza kulia) akiwa katika mtambo wa kuwekea dawa nguzo za umeme wa kampuni ya kuzalisha nguzo ya Qwihaya. Kulia kwake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Qwihaya, Leonard Mahenda.

nguzo hizo.

Alisema kuwa Serikali inategemea kuwa bei ya nguzo hizo zitapungua kutokana na kuongezeka kwa viwanda vya nguzo

ambavyo kwa sasa ni zaidi ya 11 .

Aidha alisisitiza kuhusu ubora wa nguzo zinazozalishwa nchini na uhakika wa upatikanaji

wa nguzo hizo ili kutokwamisha kazi ya usambazaji umeme.

Aidha, alisisitiza Shirika la Umeme Tanzania na Wakala wa Nishati Vijijini kuhakikisha kuwa nguzo zinazotumika kwenye miradi ya umeme zinakuwa na ubora stahiki na wahakikishe malipo ya nguzo yanafanyika kwa wakati.

Vilevile alisema kuwa mahitaji ya nguzo kwa mwaka ni takriban milioni 4.5 wakat uzalishaji ni milioni 13 hivyo hakuna visingizio vya kutokuwepo kwa nguzo nchini.

Awali, Waziri wa

Nishati pia alizindua kiwanda cha kutengeneza nguzo cha Qwihaya kilichopo katika Kijiji cha Mtwango, Wilaya ya Njombe mkoani Njombe.

Kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha nguzo 1500 kwa siku na hadi sasa kiwanda hicho kina idadi ya nguzo 400,000.

Uwepo wa kiwanda hicho umeleta manufaa kwa wakulima wa miti ya nguzo katika mikoa ya Ruvuma na Njombe kwani wanauza mazao yao kwenye kiwanda hicho.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ( Wa Tatu kutoka kulia) akifunua kitambaa kuashiria uzinduzi wa mtambo wa kisasa wa kukausha nguzo katika kiwanda kinachozalisha nguzo za umeme cha Sao Hill wilayani Mufindi Mkoa wa Iringa. Pamoja naye ni Mkuu wa Wilaya ya Mufindi Saad Mtambule ( wa Pili kushoto), Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya Sao Hill George Botther ( Wa pili kulia) na Mwenyekiti wa Bodi ya Sao Hill Godlisten Minja ( wa kwanza kushoto).



# JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



**Fika Ofisi ya Mawasiliano,**  
Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au  
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018  
**Nukushi** +255-26-2320148

[www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)

[Wizara ya Nishati](https://www.facebook.com/Wizara.ya.Nishati)

[@Nishati2017](https://twitter.com/Nishati2017)

[wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](https://www.instagram.com/wizara_ya_nishati_tanzania)

[Wizara ya Nishati](https://www.youtube.com/Wizara.ya.Nishati)